

## LUGHA YA KISWAHILI

1. Amepanga Mola wetu, kwenye dongo letu hili,  
Amegawa kila mtu, ale chake cha halali  
Iweje taifa letu, kweli kutoikubali,  
Ya kufanywa Kiswahili, Lugha ya kufundishia!
2. Lugha ya kufundishia, kutofanywa Kiswahili,  
Elimu yadidimia, kubali msikubali,  
Hadi tutapotumia, Lugha yetu ya asili,  
Elimu kwa Kiswahili, ndipo itachipukia.
3. Miongo inayoyoma, twaishia kujadili,  
Utafiti unasema, Kiswahili bilikuli,  
Matekelezo yakwama, ugumu wa serikali,  
Haitaki Kiswahili, Lugha ya kufundishia!
4. Kufunzia Kingereza, hasa wake mushikeli,  
Maana kuigeuza, kutoka Lugha ya mbali,  
Ni vigumu kuingiza, katika lugha ya pili,  
Rahisi ni Kiswahili, Lugha ya kufundishia.
5. Wanafunzi kufundishwa, kwa Kiswahili awali,  
Kingereza kughutushwa, kwenye shule za upili,  
Huko ni kutatanishwa, wambwa hawana akili,  
Utatuzi Kiswahili, Lugha ya kufundishia.
6. Ni sawa kuwafundisha, wanajeshi kwa kitali,  
Mbinu za mawe kurusha, vita watapokabili,  
Batoni ukiwashusha, zana mnazibadili,  
Hamtashinda kitali, katika mwenendo huo.
7. Kiswahili hakikidhi, kufundishia si kweli,  
Ni usemi wa maudhi, Lugha yetu twaidhili,  
Na kujishushia hadhi, chetu kua bure ghali,  
Kwa kukinza Kiswahili, Lugha ya kufundishia.
8. Si kwamba twasema tuu, kana kwamba matapeli,  
Misamiati ya juu, elimu za kila hali,  
Ni hadi Vyuo Vikuu, sayansi na tamathali,  
Kinamudu Kiswahili, Lugha ya kufundishia.
9. Kingereza kifundishwe, kwenye vyuo na skuli,  
Watoto wabidiishwe, liwe ni somo kamili,  
Na juhudi izidishwe, zaidi ya mara mbili,  
Tusemacho Kiswahili, Lugha ya kufundishia.
10. Tayari utaratibu, ulo sawa na kamili,  
Umo ndani ya vitabu, siyo kwenye mafaili,  
Si kwamba tutajaribu, hima tupeni kibali,  
Tuanzishe Kiswahili, Lugha ya kufundishia.
11. Kaditamati BAKITA, heko mnastahili,  
Endeleeni kuvuta, kamba bila ya muhali,  
Ushindi mtaupata, wa wazi si wa dalili,  
Ushindi ni Kiswahili, Lugha ya kufundishia.

*Amiri A.S. Andanenga (Sauti ya Kiza)*  
*Kinondoni-Shamba*  
*DAR ES SALAAM, Tanzania.*

---